# WAEBRANIA, MLANGO WA PILI [3]

Mlango wa 7, wa 8, wa 9, wa 10, kutoka humo ndani, loo, jamani! Shika penseli yako na karatasi, na kila kitu, tayari, kwa kuwa ninaamini Bwana atatupa wakati mzuri sana. Sasa tunaninii . . .

218 Paulo anamtukuza na kumweka, mahali Pake, Bwana Yesu. Sasa, kama tukipitia haya usiku wa leo, Jumapili asubuhi . . . Ambapo karibu haya yote yataungana moja kwa moja na Ujumbe wa Jumapili asubuhi, kwa kuwa ni "kutenganisha sabato." Hilo ni swali kubwa miongoni mwa Wasabato siku hizi. Nami ningewaalika nyote mje Jumapili asubuhi. Kwa kuwa, ni ipi iliyo sahihi, Jumamosi ama Jumapili, kwa kuabudu? Biblia inasema nini juu ya jambo hilo? Na kwa hiyo basi, endapo ninii . . . Kitabu hiki kinatenganisha torati na neema, na kinaweka kila mojawapo mahali pake. Waebrania walikuzwa kwa torati, na Paulo alikuwa akiwaambia kile neema ilifanya, pamoja na torati.

219 Sasa, hebu na tuweke tu msingi mdogo sasa. Tutaanzia nyuma.

220 Jambo lingine, nina miwani ya kusomea. Labda ninaweza . . . Kama ikitokea nitoe si—siri usiku wa leo, ninayo. Unajua mimi ni ninii sana . . . nimepungukiwa tu na miaka miwili niwe na umri wa miaka hamsini, na sioni kama jinsi nilivyokuwa nikiona, karibu nami. Wakati macho yangu . . . Nilianza kuona maneno yakiingia kiwi, nilidhani nilikuwa ninakuwa kipofu. Nikaenda kufanyiwa uchunguzi. Daktari akasema, "La. Wewe umepita tu umri wa miaka arobaini, mwanangu." Vema, akasema, kama nikiishi kuwa na umri mkubwa vya kutosha, huenda hali ya kwanza ikarudi tena, nipate kuona mbali tena. Akasema, "Sasa, unaweza ukasoma Biblia yako kama ukiisogeza mbali nawe?"

221 Nikasema, "Ndiyo."

222 Kasema, "Baada ya kitambo kidogo, mkono wako hautakuwa mrefu vya kutosha."

223 Na kwa hiyo na—natumaini sasa, katika kusoma huku, ya kwamba mimi . . . Biblia hii ndogo ya Collins ina maandishi mazuri ya herufi kubwa. Ninaweza kuisoma vizuri sana. Lakini tutakapofikia kwenye sehemu kubwa za kilindi ambapo itatupasa kuchukua Agano Jipya na Agano la Kale, na kuunganisha pamoja sehemu hizo. Nina Scofield ndogo. Nami nimezoea Biblia ya Scofield, maandishi yake ya pambizoni. Sisomi maelezo ya Scofield siku hizi, kwa kuwa sikubaliani na Scofield juu ya nadharia za—zake nyingi. Lakini ni—ninapenda jinsi ambavyo imepangiliwa, kwa sababu ina . . . Nimekuwa nayo

kwa muda mrefu, na ninaisoma, na zaidi sana, mpaka kwa namna fulani ninajua jinsi ya kupata somo langu.

224 Haya yote ni mapya kabisa kwangu, kuyafundisha, wala mimi hasa si mwalimu. Lakini, mkinivumilia kidogo, nitawaambieni Kweli kadiri ninavyoijua, hata hivyo.

225 Sasa, Kitabu hiki ni Paulo, kumbukeni. Yeye alikuwa . . . Tulimpataje? Yeye alikuwa ni mwalimu mashuhuri, kwanza, ama msomi mashuhuri. Naye alifundishwa katika Agano la Kale. Kuna mtu yeyote sasa anayeweza kuniambia ni nani tuliona alikuwa ni mwalimu wake? [Kusanyiko linasema, "Gamalieli."—Mh.] Gamalieli, mmoja wa waalimu mashuhuri sana wa zama hizo. Na halafu Paulo, tunaona, siku moja . . .

226 Kabla hajaitwa *Paulo*, kuna mtu anayeweza kuniambia jina lake lilikuwa ni nani? [Kusanyiko linasema, "Sauli."—Mh.] Sauli. Naye alikuwa ni mtu mkuu katika Yerusalemu, bingwa wa kidini. Naye alitokea kama—kama mtu wa dini aliyefunzwa vizuri sana. Aliweza kuzungumza lugha nne ama tano mbali mbali, na ni mtu mwerevu sana. Vema, je! elimu yake na akili yake vilimsaidia? La. Alisema ilimbidi kusahau yote aliyojua, kusudi amjue Kristo.

227 Kwa hiyo tunaona, basi, haihitaji mtu mwenye akili ama mtu mwerevu. Inahitaji m—mtu aliye tayari kujinyenyekeza mbele za Mungu, haidhuru vipi.

228 Je! hivi ulijua Dwight Moody alikuwa—alikuwa hana kisomo kabisa hata, kwa kweli, mwandiko wake ulikuwa mbaya sana hata sijui kama nini. Ilibidi waziandike vizuri jumbe zake, daima. Alikuwa mwenye mwandiko mbaya sana, karibu hakusoma kabisa.

229 Je! ulijua ya kwamba Petro na Yohana, wa Biblia, walikuwa hawana kisomo kabisa mpaka hata wasingeweza kuandika majina yao wenyewe, wala wasingelilijua likiwa limewekwa mbele zao? Mtume Petro, ambaye alikuwa na zile funguo za Ufalme, asingeweza kujua jina lake kama lingaliandikwa mbele zake. Wazia jambo hilo. Biblia ilisema, ya kwamba, "Alikuwa bila maarifa wala elimu." Kwa hiyo, hilo linanipa nafasi. Amina. Naam, bwana. Hilo linaingia moja kwa moja ndani, kuona kwamba Mungu angeweza kumfanyia mtu jambo hilo.

230 Sasa, pia tunaona ya kwamba, mara tu Paulo alipopata tukio kubwa . . . Ninataka kuwaulizeni. Je! ni tukio kumjia Kristo? Je! kila mtu ana tukio fulani? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Naam, bwana. Naam, bwana. Ni Kuzaliwa. Ni tukio. Na kwa hiyo tulikuwa kwenye Chuo cha Walutheri, si muda mrefu uliopita . . .

231 Nilikuwa na majaliwa alasiri ya leo, nilichelewa, nilipaswa kuwa kule saa sita, kwa ajili ya chakula cha mchana pamoja—pamoja na Tom Haire. Ni wangapi waliopata kusikia habari zake, yule shujaa mashuhuri sana wa maombi wa Kiarishi?

Naye amekuwa pamoja na Ndugu huyu Epp, kwenye kipindi chake, na anahudhuria sehemu nyingi hapa Marekani. Nami nilikula chakula cha mchana naye leo. Nasi tulikuwa... Nilikuwa nimechelewa kwa saa tatu hivi. Ilikuwa yapata saa tisa na nusu, saa kumi kasorobo, tulipokula. Lakini ilikuwa ni sawa. Nasi tulikuwa tukizungumzia juu ya mambo haya, juu ya jinsi ambavyo Yesu Kristo ndiye Kichwa cha mambo yote.

232 Sasa, wakati Paulo alipotambua jambo hili, alipata ujuzi huu. Na ndipo kabla hajalikubali tukio hili, halina budi lichunguzwe kwa Biblia. Nasi tunaona ya kwamba yeye—ya kwamba yeye aliondoka akaenda katika taifa lingine, na huko akakaa kwa muda wa miaka mitatu, akiyachunguza Maandiko, kuona kama tukio lake lilikuwa ni la kweli.

233 Sasa, tunatambua ya kwamba alikuwa na jambo zito la kukabiliana nalo. Ilibidi arudi na kuliambia kanisa lake, watu wote, mambo yale yale aliyokuwa akiyatenda mabaya yalikuwa ni ya kweli.

234 Je! ilikubidi kufanya kitu kama hicho? Hakika, karibu wote walifanya vivyo hivyo, ilibidi kurudi nyuma na kusema, "Hao watu tuliowaita 'watakatifu wanaojifingirisha,' tumekuja kutambua, walikuwa wakisema kweli." Unaona? Jambo ndilo hilo. Ilibidi tu tugeuke. Na mambo yale ambayo tuliyachukia hapo nyuma, sasa tunayapenda. Ni kuongoka, jambo geni.

235 Aha! Nilifanya tamshi hilo, la "watakatifu wanaojifingirisha." Hakuna kitu kama hicho. Hakuna kitu kama hicho. Lakini, wanawaita watu namna hiyo, watu wa utakatifu. Lakini hakuna watakatifu wanaojifingirisha. Hakuna kitu kama hicho. Hakuna taarifa ya kanisa lolote lililopata kuandikishwa namna hiyo, kadiri niwezavyo kuona mimi, kati ya madhehebu mia tisa sitini na kitu mbali mbali. Hakuna dhehebu kama mtakatifu anayejifingirisha. Ni ji—jina tu ambalo Ibilisi alilibandika kwa Kanisa.

236 Lakini wanawaita hao, katika siku hizo...Ni wangapi wanaojua kile walichowaita katika siku za Paulo? Wazushi. Unajua maana ya *mzushi*? "Mwenda wazimu." Ni wenda wazimu. Kwa hiyo, ni afadhali mara moja niitwe "mtakatifu anayejifingirisha" kuliko "mzushi." Nawe je? Kwa hiyo kama wao—kama waliitwa hivyo, na wakafurahi!

Na Yesu alisema kwamba tufanye nini juu ya jambo hilo? Alisema, "Furahini, na kushangilia sana; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa Mbinguni, kwa kuwa ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa mbele yenu." Walifanya jambo hilo.

237 Akasema kuninii, "Shangilieni mno." Chochote cha *mno* ni "kilichoinuliwa juu sana," chenye furaha sana. Nao wanafunzi, walipohesabiwa wanastahili kuchukua shutuma za Jina la Yesu, walifurahi kwa furaha kuu ya kwamba waliweza kuchukua shutuma za Jina Lake.

238 Na siku hizi, watu wengi siku hizi, kama ingetokea waitwe mtakatifu anayejifingirisha, wangeona soni, "Jamani! Labda nilikosea, kwa kuanzia."

Lakini wao walifurahia jambo hilo, "Loo, jamani, kulichukua Jina hilo!"

239 Na sasa, katika karne ya pili, waliwaita "*misalaba-migongoni*." Hapo ndipo Wakristo walipokuwa wakibeba msalaba mgongoni mwao, kuonyesha ya kwamba walisulibiwa pamoja na Kristo. Wanawaita "*misalaba-migongoni*." Sasa ninajua Wakatoliki wanajiita hivyo, bali hilo halikuwa ni kanisa Katoliki. Lilikuwa ni kanisa la Kiprotestanti kabla halijaitwa kanisa la Kiprotestanti. Halikuwa likipinga chochote ila dhambi. Sababu ya kuitwa kanisa la Kiprotestanti siku hizi ni kwa sababu lilipinga fundisho la sharti la—la Kikatoliki. Lakini ni ninii . . . Hilo, lingali, lilikuwa halijafanyika dhehebu wakati huo, wakati walipoitwa *msalaba-mgongoni*.

240 Hebu chukua tu historia ya Josephus na waandishi wengine, na *Babiloni Mbili* kilichoandikwa na Hislop, na kadhalika, nawe utaona ya kwamba hiyo ni kweli, ya kwamba hawakuwa ni kanisa. Kanisa la kwanza lililowahi kuunda dhehebu, lilikuwa ni kanisa Katoliki, yapata miaka mia tatu, kwenye kipindi cha—cha wale mitume wa mwisho. Yapata miaka mia tatu baadaye, kanisa Katoliki liliunda dhehebu. Ndipo mateso yakaanza, na kuwalazimisha watu kuingia katika kanisa Katoliki, nao waliunganisha kanisa na serikali.

241 Hiyo ilikuwa ni baada, ya kile kilichoitwa, kuongoka kwa Konstantino, kutoka upagani akaingia Ukatoliki. Lakini, kama mtu yeyote alipata kusoma historia yake, yeye hakuwa ameongoka, mambo yale aliyofanya. Loo, jamani! Jambo pekee alilopata kufanya la kidini lilikuwa ni kuweka msalaba kwenye kanisa la Mt. Sofia. Hilo ndilo jambo pekee alilopata kufanya, kujifanya hata yeye ni wa kidini. Alikuwa mwo—mwovu. Bali wao wanakuita huko ni kuongoka kwa—kwake. Karibu kunalingana na baadhi ya kunakoitwa kuongoka kwa siku hizi.

242 Sasa, lakini, tunaona, wakati Paulo alipoongoka na akapata tukio hili halisi, yeye aligeuzwa kabisa.

Na, unajua, *kuongoka* maana yake ni "kugeuzwa." Unaenda upande *huu*, kisha unageuka na kuanza kurudi hivi. Naam, bwana. Ni kugeuka, kupinduka kabisa.

243 Naye Paulo, mara alipoongoka, kabla hajaweza kamwe kulifanya tukio lake . . . Sasa, yeye alikuwa na tukio la ajabu.

Sasa, ninaamini, wakati unapomkubali Kristo, kama tu Mwokozi wako binafsi, ni tukio. Ninaamini, furaha ya kujua dhambi yako imesamehewa, kunauchangamsha tu moyo wako, kupindukia.

244 Lakini basi wakati Roho Mtakatifu mbarikiwa anaposhuka, hilo ni tukio, huko ni Kuzaliwa Upya, ambako kamwe hutasahau. Unakuwa Mtoto wa Mungu. Na hicho ndicho kinachosababisha jambo hilo.

"Unajuaje jambo hilo, Ndugu Branham?"

245 Sasa, haya ni masomo ya kufundisha. Watu wengi, Wamethodisti, wanajaribu kusema, "Walipiga makelele walipompata." Vema, hilo ni sawa. Kama ulimpata, na ukapiga makelele, sawa. Ati kwa sababu ulipiga makelele, haikuwa ni ishara ya kwamba ulimpata, maana wengi walipiga makelele wala hawakumpata.

246 Wapentekoste walisema, "Walinena kwa lugha, walimpata." Hilo ni sawa. Kama ulinena kwa lugha, na ukampata, sawa. Bali ungaliweza kunena kwa lugha na bado usimpate. Kwa hiyo?

247 Kwa hiyo, unaona, hata hivyo, ni tukio la kupita toka mautini kuingia Uzimani; wakati mambo yote ya kale yanapokufa, na mambo yote yanakuwa mapya. Kristo anafanyika halisi. Mambo ya kale yanaanguka, mashina ya kale ya tamaa za kimwili. Unajua jinsi ya kuchimbua shina litoke? Tulikuwa tukichukua jembe la kuchimbua na kuanza tu kazi, na kulichimba mpaka hapakuwapo na chembe yake iliyosalia. Nao walisema, "Shina lolote la uchungu likichipuka ndani yako, ling'oeni." Hiyo ni kweli. Na hilo ndilo ambalo Roho Mtakatifu hufanya, hung'oa mizizi yote. Anaichimbua. Anailundika; anaichoma moto. Anaitupilia mbali. Ndipo unapata zao zuri, kama tukifanya hivyo.

248 Sasa, Paulo alijua ya kwamba jambo fulani lilitukia, kwa hiyo anashuka kurudi kwenda huko Arabuni, na huko anachunguza kwa miaka mitatu manabii wote wa Agano la Kale, jinsi walivyotabiri. Naye akaja kupata kuona ya kwamba ilikuwa ni Kweli tupu.

249 Sasa, linganisha hilo na siku hizi, unaona, juu ya tukio hili tulilokuwa nalo hapa kwenye kanisa hili dogo: la Nyota ya Asubuhi ikitokea kule, ile Nuru kuu iliyoshuka, ambayo ingetabiri na kuonyesha mambo yatakayotukia. Mwajua, hilo ni ajabu sana. Lakini ndugu yangu mhudumu aliniambia, "Lilikuwa ni la Ibilisi." Wala mimi—mimi nisingeweza kufahamu jambo hilo.

250 Kwa hiyo, sikusema neno juu yake mpaka usiku mmoja, kulikuwako na tukio lililotukia huko Green Mill, Indiana, wakati Malaika wa Bwana alipokuja akitembea sakafuni na akasimama pale, na kulithibitisha jambo hilo kwa Maandiko. Ndipo hilo likawasha moto. Ndipo ukaanza kusambaa.

251 Na si zaidi ya Jumapili iliyopita, tuliona alama zisizokosea za Yesu Kristo, ambaye anaweza kumchukua mtu ambaye hajatembea, wala hakuninii. . .Neva yake ya mlingano imekwisha, wakati akina Mayo na madktari walio bora sana

waliposema, "Imekwisha, maisha." Naye ameketi akiwa kipofu; akasimama na akatoka jengoni, akisukuma kiti chake cha magurudumu na kushuka kwenye vipandio, angeweza kutembea na kuona kama mtu mwingine yeyote. Hiyo inaonyesha ni nguvu za Bwana Yesu aliyefufuka. Hilo hapo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

252 Hivyo basi sisi si ni kundi lililo na furaha usiku wa leo, tukijua ya kwamba Mungu amethibitisha tukio hili kuu tulilo nalo, kulinganishwa na Biblia Yake na pamoja na hizo ahadi? Kwa hiyo inatupasa kuwa na furaha sana. Nasi tunatambua basi, ya kwamba katika mlango wa pili, tunaona, "Hatupaswi kuacha mambo haya . . . Hatupaswi kutoyajali mambo haya." Tunapaswa kuyashikilia sana mambo haya.

*Basi tutapataje kupona, tusipoujali wokovu mkuu kama huu; . . .*

253 Tutafanya nini, kwa kuzingatia Neno la Mungu, tutakaposimama Hukumuni? Huwezi kusema, "Mimi sikujua vinginevyo." Loo, naam, ulijua. "Vema, sasa, Ndugu Branham angeweza kuwa alikosea." Hiyo ni kweli. Bali Mungu hana makosa. Neno Lake halijakosea." Na hebu wazia tu, juu ya jambo lile lile, Biblia, ambayo wakati mmoja ilikuwa hai katika mitume, wanaishi tena. Loo, Jina la Bwana lihimidiwe!

254 Ninapowazia ya kwamba nina umri wa miaka arobaini, nikikaribia hamsini, na siku za ujana wangu zimekwisha, na kadhalika; kujua ya kwamba tangu nilipokuwa mvulana mdogo ya kwamba nilikuwa na Ahadi hii iliyobarikiwa, nami nimeitangaza kwa ndugu zangu na dada zangu; na kuona kabisa maelfu ya wale waliotoka gizani, kujua ya kwamba tunaenda kwenye Makazi yetu ya Milele, kwa waliobarikiwa. "Na kama maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa," kabla sijamaliza kuhubiri, "kuna moja inayoingojea huko ng'ambo kwa ajili yake." Haleluya! Kujua ya kwamba kuna idadi kubwa ya watu wanaoketi hapa, ambao, kama wangeyaacha maisha haya sasa hivi; kabla hatujaweza kupeleka miili yao kwa mzishi, wangekuwa katika ule mwili wa utukufu huko ng'ambo, wakifurahi pamoja na watakatifu wa Mungu, wakiwa tayari katika Uwepo wa Mungu, wapate kuishi milele. Wakiwa na thibitisho kamilifu kabisa kwamba ni jambo halisi! Amina.

255 Loo, hilo lingemfanya Mpresbiteri kupiga makelele! Waliyapiga Jumapili, sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hao watu walikuwa ni Wapresbiteri. Bila shaka wangepiga, kuwazia hilo. Loo, si ajabu watu wanashikwa na mhemuko! Mbona, kama ukishikwa na mhemko kutokana na kupiga mpira ama kutupa mmoja uingie kwenye kikapu, ni zaidi sana vipi itakufanya ushikwe na mhemuko kujua ya kwamba umepita toka mautini ukaingia Uzimani, ya kwamba wewe ni Kiumbe kipya katika Kristo! Unajua hilo kulingana na vile roho yako

inavyokuongoza mbali na kijicho, na hila, na uadui, na mambo yote ya dunia. Na moyo wako daima umeelekea kwa Kristo. Hayo ndiyo makusudio yako. Hayo tu ndiyo unayofikiria niani mwako, moyoni mwako, siku nzima na usiku kucha. Unapoenda kitandani kulala usiku, na kuweka mikono yako nyuma yako, namna *hii*, na unalala tu pale na kumsifu mpaka unashikwa na usingizi. Unaamka, asubuhi, ungali unamsifu. Amina. Loo, jamani!

256 Nimejaribu kumsifu. Kila asubuhi tumekuwa tukiamka saa kumi, Mimi pamoja na Ndugu Woods, tukitoka asubuhi na mapema, kwenda kuwinda kindi. Ninamsifu chini ya kila mti, ninaamini, ninaoufikia. Siwezi kuona mti, bila kumsifu. Nawazia, Yeye aliukuza huo mti. Unamwona maskini panzi mdogo akiruka juu; Yeye anamjua panzi huyo. "Loo," unasema, "upuuzi, Ndugu Bill." Loo, la, sivyo. Yeye anajua kila mahali alipo kindi. Anajua mahali kila kipepeo alipo.

257 Mbona, wakati mmoja, Yeye alihitaji fedha kidogo, na akasema, "Petro, kuna samaki, muda kidogo uliopita, aliyemeza sarafu, ya kutosha tu, kiasi tunachohitaji. Nenda ukatupe ndoana ndani. Nitamtuma kule. Toa sarafu hiyo mdomoni mwake, maana hawezi kuitumia, yeye mwenyewe. Nenda ukamlipe fungu letu la kumi na kodi." Amina.

258 Na majuma machache yaliyopita, niliona samaki mdogo ameuawa, anaelea majini. Ninyi nyote mlisikia hadithi yake. Yule pale Ndugu Woods, na ndugu yake na hao wengine hapa kushuhudia jambo hilo. Samaki huyo mdogo amelala mauti kwa nusu saa, juu ya maji, huku matumbo yake yametokeza mdomoni mwake. Ndipo Roho Mtakatifu aliye mkuu akashuka, baada ya Yeye kusema, siku moja iliyotangulia, "Utaona ufufuo wa mnyama mdogo." Na kesho yake asubuhi yapata, punde kidogo baada ya mapambazuko, tulimwona huyo samaki mdogo, si mrefu zaidi ya *hivi*. Wakati Roho wa Bwana aliposhuka, na kusema, "Ewe samaki mdogo, Yesu Kristo anakufanya mzima." Na samaki huyo aliyekufa, alikuwa akielea juu ya maji kwa karibu nusu saa, akawa mzima na akaenda zake akiogelea upesi tu alivyoweza. Loo, jina la Bwana lisifiwe. Jinsi Yeye alivyo wa ajabu!

259 Si ajabu Paulo angeweza kusema, ya kwamba, "Alikuwa katika mfano wa Melkizedeki." Yeye alikuwa ni Melkizedeki. "Melkizedeki hakuwa na mwanzo wa siku zake. Hakuwa na mwisho wa miaka. Hakuwa na mwanzo wa maisha wala mwisho wa uhai. Hakuwa na baba wala mama." Kwa hiyo, Yeye asingeweza kuwa ni mtu mwingine yeyote. Yeyote aliyekuwa, Yeye angali yu hai usiku wa leo. Kwa hiyo, Yeye ndiye pekee namna moja ya Uzima wa Milele, na huo ni wa Mungu.

260 Jana jioni tulipokuwa na majadiliano, ndugu fulani hakuweza kuelewa na utatu wa Mungu, na jinsi tulivyokuwa

tukizungumzia kuhusu jambo hilo. Jinsi ambavyo Yesu alisimama pale, Mwanadamu, wa umri upatao miaka thelathini. Naye akasema . . .

Wao walisema, "Loo, baba zetu walikula mana jangwani."

261 Akasema, "Nao, hao wote, wamekufa." Lakini akasema, "Mimi ndimi hicho Chakula cha Uzima kishukacho kutoka kwa Mungu Mbinguni, ambacho mtu hula wala hafi."

262 "Loo," wakasema, "baba zetu waliunywea ule Mwamba jangwani."

263 Akasema, "Mimi Ndimi Huo Mwamba." Mtu wa umri wa miaka thelathini. Kasema, "Ibrahimu alishangilia kuiona siku Yangu."

264 "Mbona," akasema, "sasa unataka kuniambia ya kwamba Wewe ni wa rika ya Ibrahimu, na hujapata umri wa miaka hamsini bado, na unataka kusema ya kwamba umemwona Ibrahimu ambaye amekufa kwa mika mia nane? Tunajua ya kwamba Wewe una pepo sasa. Una kichaa." Hivyo ndivyo . . . Hiyo ndiyo maana ya *pepo*, mtu mwenye "kichaa." Wakasema, "Una pepo, na una wazimu."

265 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO."

266 Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Yeye hakuwa mwanadamu tu, wala hakuwa nabii tu. Yeye alikuwa Mungu, Mungu akiishi duniani katika mwili wa nyama ulioitwa "Yesu," Mwana wa Mungu aliye—aliyefanyika mwili. Hivyo ndivyo hasa alivyokuwa.

267 Sasa, tunamwona hapa, kwamba katika sehemu ya mwisho sasa, ya kumalizia kwa mlango wa 2, ambao ninataka kuufikia, kuanzia kwenye kifungu cha 16, ama kifungu cha 15.

> *Akawaacha* huru *wale . . . maisha yao yote kwa hofu ya mauti—ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.*

Hivyo ndivyo alivyosema ya kwamba Yesu alifanya, kwamba alikuja kuwaweka huru na utumwa, ambao maisha yao yote walihofu mauti.

268 Sasa hakuna haja ya kuhofu mauti. Sasa, hakuna budi, tunahofu; sisi, hakuna hata mmoja wetu anayetaka kufa, tunakoita, *kufa*. Lakini je! unajua ya kwamba kama mtu amezaliwa mara ya pili hawezi kufa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Anawezaje kuwa na Uzima wa Milele na kisha afe? Hawezi kufa. Kitu pekee ambacho ni mauti, Neno *mauti*, maana yake ni "kutenganishwa." Sasa yeye atatengwa mbele ya macho yetu. Lakini yeye daima yuko katika Uwepo wa Mungu, na daima atakuwa. Kwa hiyo, kifo si kitu kigumu. Mauti ni kitu cha utukufu. Mauti ndiyo yanayotupeleka katika Uwepo wa Mungu.

269 Lakini sasa, bila shaka, sisi, tukiwa wanadamu, tunatembea katika mazingira haya yenye giza hapa, ha—hatufahamu jambo hilo jinsi tunavyopaswa kufahamu. Na, hapana budi, wakati maumivu makali sana ya mauti yanapokuja, yanamfanya aliye mtakatifu sana wetu ahofu na ayakatae. Yalimfanya Mwana wa Mungu kusema, "Je! kikombe hiki kingeweza kunipita?" Ni kitu cha kutisha sana. Usilichukue vibaya. Kwa sababu sisi. . .Ni mshahara wa dhambi, ndivyo mauti ilivyo, nayo hayana budi kuwa ni mabaya sana.

Bali kama tunaweza tu kuangalia ng'ambo tu ya pazia, huko ng'ambo, huko ndiko kwenye mambo. Jina la Bwana lihimidiwe! Ng'ambo tu ya pazia, huko ndiko mwanadamu anapenda kuangalia usiku wa leo. Maskini Anna Mae Snelling na hao wengine walikuwa wakiimba wimbo fulani hapa, "Bwana, Nijalie Niangalie Ng'ambo ya Pazia la Wakati." Kila mtu anataka kuona huko.

270 Sasa, ndio sasa tuko, katika kifungu cha 16. "Maana hakika alitwaa . . . "

> *Maana ni hakika, hajitwalii asili ya malaika, ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu.*

271 Loo, tunataka kushikilia jambo hilo tena sasa. Sasa tunashuka moja kwa moja kupata . . . Maana, sehemu ya kwanza ya mlango huu wa 3, sehemu yake ya mwisho, inaungana na "siku ile kwa ajili ya sabato," kwa ajili ya Jumapili hii ijayo.

272 Sasa angalia.

> *. . .hajitwalii asili ya malaika;. . .*

Sasa, ni nani "Huyu," ambaye anazungumza habari Zake? Kristo. Kristo ni nani? Mungu, yule Logos wa Mungu.

273 Sasa hebu nielezee jambo hili tena, mpate kuwa na hakika. Mungu si Miungu watatu. Utatu wa Mungu ni Mmoja. Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, haimaanishi kuna Miungu watatu mbali mbali. Kama wapo, sisi tungekuwa makafiri. Hiyo ndiyo sababu Wayahudi hawawezi kuelewa. Kamwe hilo halijawahi kufundishwa katika Biblia. Sasa, linafundishwa katika kanisa Katoliki, kweli kabisa, huko ndiko ambako ubatizo wa utatu ulikotoka.

274 Huko Afrika wanakubatiza mara tatu kifudifudi: mara moja kwa ajili ya Mungu Baba; mara moja kwa ajili ya Mungu Mwana; mara moja kwa ajili ya Mungu Roho Mtakatifu. Sasa, hilo ni kosa. Hakuna mafundisho ya namna hiyo katika Biblia. Unaona?

275 Na sasa, hivyo—hivyo ndivyo walivyofundisha. Yalikuja kupitia kwa Luther; kutoka kwa Luther, yakaingia kwa Wesley; moja kwa moja kupitia katika nyakati kadiri zinavyoendelea. Bali kamwe halikuwa ni fundisho la Biblia. Daima limekuwa ni kosa, tangu lilipoanzishwa.

276 Sasa, kwa hiyo, Mungu alikuwako hapo mwanzo. Kabla hakujakuwako na nuru yoyote, kabla hakujapata kuwako na atomi yoyote, kabla hapajakuwako na nyota, kabla hakujakuwako na kitu chochote kinachoonekana, Mungu alijaza anga lote. Na Humo ndani hamkuwamo na kitu ila usafi; upendo msafi, utakatifu msafi, haki safi. Ilikuwa ni Roho. Yeye alifunika anga zima lote kutoka Umilele, ambapo hatuwezi kuliwazia Hilo. Limezidi kitu chochote ambacho tungeweza kuwazia.

277 Ni kama kupitia kwenye darubini ile, tungeweza kuona umbali wa mwendo wa nuru angani wa miaka milioni mia—mia moja na kitu. Wazia jambo hilo. Eneo la anga la mwendo wa nuru wa miaka milioni mia moja. Na nuru—nuru inaenda mbio za kama maili elfu nane kwa sekunde moja. Nao mwendo wa nuru wa maili za anga milioni mia moja . . . Hebu wazia tu hizo zingekuwa ni maili milioni ngapi. Usingeweza hata kuzihesabu. Unaweza tu kuchukua safu ya tisa-tisa na kuizungusha Jeffersonville, na hata hivyo usingeweza kuziweka katika maili za maili. Hebu wazia. Na mbele ya hizo kungali kuna nyota na sayari. Na Mungu, kabla haijakuwapo moja ya hizo, Yeye alikuwapo. Unaona?

278 Na sasa Logos aliyetoka kwa Mungu, ambaye alikuwa ni yule Lo—Logos, yote haya yalianza kufanyika katika umbo la mwi—mwili. Na umbo hili la mwili liliitwa, katika fundisho la mwanachuoni, Logos, yule Logos aliyetoka kwa Mungu. Kwa maneno mengine, ne—neno zuri zaidi kwake, lilikuwa ni ule tunachoita thiofania. (Thiofania ni mwili wa binadamu uliotukuzwa.) Si hasa wenye mwili na damu kama utakavyokuwa katika kipindi chake cha kutukuzwa, bali ni wa umbo la mwili wa mwanadamu ambao hauli, wala haunywi, bali ni—ni mwili, mwili unaotungojea mara tutakapouacha huu. Sasa, humo, tunaingia katika mwili huo. Naye Mungu alikuwa katika mwili wa jinsi hiyo, kwa kuwa Yeye alisema, "Na tumfanye mtu mfano wetu na sura yetu."

279 Sasa, mtu alipoingia katika mwili huo, alikuwa na utawala juu ya samaki wote, na ndege, na—na wanyama wa kondeni. "Na halafu hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi," Mwanzo 2. Yeye alikwisha kumfanya mwanamume na mwanamke, bali hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi.

Basi Mungu akamfanya mtu kutoka katika mavumbi ya ardhi. Akampa mkono kama wa—wa sokwe mtu. Akampa mguu kama wa dubu. Akampa, akamfanya, kwa sura hiyo. Na mwili huu wa dunia hii uko katika mfano wa mnyama, na umefanywa kwa vitu vya namna ile ile. Mwili wako umefanywa kwa vitu vile vile kama farasi, au mbwa, ama kitu kama hicho. Umefanywa kwa kalisi, potashi, petroli, nurulimwengu. Wewe si ninii tu . . . Nyama yote kama hiyo si nyama ya namna ile ile; ni nyama tofauti, bali imefanywa kwa mavumbi ya ardhi mahali ilipotoka.

Lakini, tofauti kati ya mnyama na mwanadamu, Mungu aliweka nafsi katika mwanadamu, wala hakuiweka katika mnyama. Kwa sababu, nafsi iliyokuwa katika mwanadamu ni ile thiofania

Loo, kamwe si—si-, sitafikia kamwe kwenye. . .somo hili, bali sina budi kupata hili.

280 Angalia. Hivi hukumbuki wakati Petro alipokuwa gerezani, naye Malaika wa Bwana akaja na akaifungua ile milango?

281 Tulikuwa tukipitia kwenye soko hili kuu hapa, hivi majuzi, ndipo mlango ukafunguka mbele zetu. Nikasema, "Unajua, Biblia ndiyo iliyokuwa ya kwanza kuwa na kitu hicho." Unaona? Sasa, mlango unajifungua wenyewe.

282 Ndipo wakati Petro alipotoka, akipita karibu na wale walinzi, walikuwa vipofu kwake. Alipita mlinzi wa ndani, mlinzi wa nje, akatoka barazani, akapita ukutani, akatoka akaingia barabarani. Wala hakuna mmoja wao alijua kwamba alikuwa ni nani. Wala hakujali. . .walidhani alikuwa ni mlinzi mwingine ama yeyote yule. Wao. . .Alipita tu pale, ndipo mlango ukajifungua wenyewe, alipokuwa akitoka, kisha ukajifunga nyuma yake. Ndipo wakati alipotoka huko nje, alidhani alikuwa anaota. Ndipo aliposhuka akaenda kwenye nyumba ya Yohana Marko, ambako walikuwa na mkutano wa maombi. Ndipo alipokuwa akipiga hodi. . .[Ndugu Branham anagonga mimbara. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .kuwa miongoni mwenu.

283 Loo, Yeye ni mtukufu. Yeye ni wa ajabu.

> Sasa, Loo, yeye hakufanywa katika mfano wa malaika; *ila atwaa asili ya mzao wa Ibrahimu. Mungu alifanyika mzao wa Ibrahimu.*

284 Sasa, kama tungalikuwa na wakati, kurudi nyuma na kuonyesha jinsi alivyofanya jambo hilo katika Agano! Mmenisikia nikihubiri juu ya jambo hilo, mara nyingi, jinsi ambavyo yeye aliwachukua hao wanyama na akawapasua, kisha akatupa hua na njiwa ndani. Kisha akaangalia, akaona moshi mdogo, tisho jeusi, mauti. Halafu, akaona tanuru inayotoka moshi, kuzimu. Lakini, ng'ambo ya hayo, kuliondoka nuru ndogo nyeupe. Na hiyo ndogo nyeupe ilipitia katikati ya kila kipande cha dhabihu hiyo iliyokatwa, ikionyesha ya kwamba hivyo ndivyo atakavyofanya. Ndipo akaapa kiapo, wakati alipofanya hivyo, kisha akaandika Agano, akionyesha ni kitu gani atakachofanya.

285 Naye, Yesu Kristo, alikuja duniani; Mungu, *Imanueli*, "Mungu katika mwili." Na hapo Kalvari, Yeye aliraruliwa. Ndipo Roho Yake ikarudi kwenye Kanisa. Na mwili Wake ukainuliwa na kuwekwa kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu.

Kiti cha Enzi cha Mungu! Yule aliye kwenye Kiti cha Enzi ni Hakimu. Tunajua jambo hilo. Vema, Hukumu iko wapi? Baba ametoa. . . Yeye hamhukumu mtu yeyote. Bali Baba amempa Mwana hukumu yote. Kwa hiyo Yeye ni. . . Na Uhai Wake ni Kuhani Mkuu, aliyeketi pale pamoja na mwili Wake mwenyewe, kama dhabihu, kufanya dua kwa ajili ya maungamo yetu. Amina. Ndugu, hilo linaweka jambo fulani ndani yako.

286 Angalia, "Yeye alichukua Uzao wa Ibrahimu." Alifanyika Mwanadamu. Mungu, aliyefanyika mwili miongoni mwetu, apate kutukomboa. Katika maneno mengine, Mungu alifanyika dhambi, ili kwamba sisi wenye dhambi tupate kuwa washiriki Wake. Na wakati tunaposhiriki pamoja Naye, tunashiriki ninii Yake. . . Sisi tulikuwa watu wa wakati, sabini. Ndipo Mungu akashuka akafanyika mmoja wetu, sabini, kwa ajili ya wakati Wake uliokusudiwa, tupate kushiriki Uzima Wake wa Milele. Ndipo wakati tunapozaliwa mara ya pili, sisi ni wana na binti za Mungu, nasi tuna Uzima wa Milele, wala hatutaangamia kamwe.

Loo, ni Mwokozi wa kuhimidiwa na—na—namna gani! Loo, hakuna njia ya kuandika jambo hilo. Hakuna njia ya kulielezea. Halielezeki kabisa. Hakuna mtu anayeweza kuelezea jinsi lilivyo kuu. "Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu!" ni kweli.

> *Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote*. . . (Wazia jambo hilo.). . . *apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu,*. . . (Sikilizeni jambo hili). . . *ili afanye suluhu*. . . *dhambi za watu wake.*

Kupatanisha, sasa, Mungu, akijua haki, ilibidi afanyike asiye na haki, apate kuhisi jinsi ilivyo kuwa mwenye dhambi, apate kurudi akafanye upatanisho, kwa njia ya "upatanisho," na apate kuwarehemu watu.

287 Kifungu kinachofuata, sikilizeni Hicho hapa.

> *Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa*. . .

288 Mungu asingeweza kuteseka katika Roho. Ilibidi afanyike mwili, apate kusikia uchungu wa magonjwa, apate kusikia jaribio la tamaa mbaya, kusikia jaribio la kupungukiwa, kusikia jaribio la njaa, kusikia nguvu za mauti. Apate kutwaa juu Yake jukumu la kusimama Mbele ya Roho Yehova mkuu, yule Roho, si Mwanadamu; Roho, kufanya upatanisho kwa ajili ya maisha haya. Basi Yesu alichukua hayo, kusudi apate kutupatanisha, kwa maana anajua jinsi hali ya mambo ilivyo. Unapokuwa mgonjwa, Yeye anajua unavyojisikia. Unapojaribiwa, Yeye anajua unavyojisikia.

289 Sasa, je! umepata kuona wakati tunapompigia kura rais, kila mkulima atampigia kura rais ambaye amekuwa mkulima,

kwa maana anajua sehemu iliyo ngumu ya maisha ya mkulima. Unaona? Mtu anataka mtu fulani anayeelewa.

290 Na kabla Mungu hajafahamu; Yeye akiwa ule Utakatifu mkuu. Angewezaje kupata kufahamu, baada ya kumhukumu mwanadamu? Kwa utakatifu Wake, Yeye alimhukumu mwanadamu. Na njia pekee atakavyopata kujua jinsi ya kumhesabia haki mwanadamu ni kufanyika mwanadamu.

291 Ndipo Mungu akamtia uvuli bikira naye akazaa mwili, si damu ya Kiyahudi, si damu ya Mmataifa, bali Damu Yake Mwenyewe. Damu ya Mungu iliyoumbwa, bila kujuana kimwili hata kidogo, hata kidogo, pasipo na tamaa ya kujuana kimwili. Na Chembechembe hii ya Damu, iliyoumbwa katika tumbo la uzazi la mwanamke huyu, ilimleta Mwana. Na wakati alipokuwa akibatizwa na Yohana Mbatizaji, Yohana alisema, "Ninashuhudia, kuona Roho wa Mungu (kama hua) akishuka na kukaa juu Yake."

292 Si ajabu Yesu aliweza kusema, ya kwamba, "Mamlaka yote ya Mbinguni na duniani yamewekwa mkononi Mwangu." Mungu na Mwanadamu wakawa Mmoja. Mbingu na nchi zilikumbatiana, Naye alikuwa Ndiye anayeweza kuleta upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Hiyo ndiyo sababu kwamba, katika Jina Lake, uponyaji unafanyika. Yeye anajua maumivu yako.

293 Je! umewahi kusikia wimbo huu mfupi wa kale?

> Yesu anajua uchungu unaosikia, Yeye anaweza kuokoa na anaweza kuponya;
> Upeleke mzigo wako kwa Bwana na uuache pale.

Hiyo ni kweli. Yeye anajua

> Wakati mwili wetu unateseka kwa uchungu, wala hatuwezi kupata afya tena,
> Kumbuka tu Mungu Mbinguni hujibu maombi;
> Yesu anajua uchungu unaosikia, Yeye anaweza kuokoa na anaweza kuponya;
> Upeleke tu mzigo wako kwa Bwana na uuache pale.

294 Hayo tu ndiyo anayokusihi, "Uache tu pale." Kwa nini? Yeye ndiye Kuhani wetu Mkuu anayesimama hapa, anayejua jinsi unavyokuambia. Naye anajua jinsi ya kukupatanisha uirudie neema, na jinsi ya kukurejeshea afya yako. Anajua yote juu ya jambo hilo; Yeye aliteseka. Wakati huna mahali pa kulaza kichwa chako; Yeye naye alikuwa na jambo hilo. Unapokuwa na nguo moja tu ya kubadilisha; Yeye naye alikuwa vivyo hivyo. Unapodhihakiwa, unapoteswa, Yeye alikuwa na yayo hayo.

295 Sikilizeni kifungu cha mwisho sasa. Vema.

. . .*aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.*

Ama, kwa maneno mengine, Yeye anaweza *kuwahifadhi* wao, *kuwapa msaada* wao, kuwafanya wao. . .*kuwahurumia*. Kwa sababu, Mungu Mwenyewe alifanyika mtu, kusudi apate kuuhisi.

296 Kumbukeni, hivi majuzi usiku, hivi hatukufundisha juu ya jambo hilo? Jinsi ambavyo ilimbidi Mungu kuninii. . .Mauti yalikuwa na mwiba ndani yake, tishio ndani yake. "Siku zao zote walikuwa katika utumwa kuhusu *mauti* haya." Ndipo Yesu akaja, apate kuondoa huo mwiba kutoka katika mauti.

Ndipo alipokuwa akipanda mlimani, je! mnakumbuka jinsi tulivyolielezea jambo hilo? Hayo madoa madogo mekundu kwenye koti Lake, baada ya kitambo kidogo yote yalifanyika doa moja kubwa, na kumwaga Damu karibu Naye. Maskini mwili Wake mnyonge, asingeweza kwenda mbele zaidi, naye akaanguka. Simoni Mkirene, yule mtu mweusi, alimsaidia kuubeba msalaba juu ya kile kilima.

Ndipo wakati walipomsulibisha msalabani, Naye akapiga makelele apate maji. Mtu yeyote anayetokwa na damu hupatwa na kiu cha maji.

297 Mnakumbuka nilipohubiri hivi majuzi usiku juu ya "Kulungu na ayala wanaokionea kiu kijito cha maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu"? Kama kulungu amejeruhiwa na ni mzima, akimwagika damu, hana budi afikie kwenye maji la sivyo atakufa.

298 Nilipigwa risasi, huko kondeni, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na minne. Nami nilikuwa nimelala pale. Miguu yangu ilikuwa imelipuliwa juu yangu, kama sambusa, kutokana na bunduki ya geji kumi na mbili. Ndipo nikalilia maji ya kunywa, "Jamani, nipeni maji ninywe!" Nilikufa ganzi, mdomo wangu ulikufa ganzi.

299 Rafiki yangu msiri alikimbilia kwenye kidimbwi cha zamani, kilichokuwa na kila namna ya vifurukuta mikia, kinamasi. Sikujali kilikuwa na nini. Naye akaijaza maji, nami nikafungua mdomo wangu, ndipo akaikamua kofia yake kabisa namna hiyo, mdomoni mwangu. Mtu ilibidi upate maji unywe.

300 Alikuwa akitokwa na damu. Akasema, "Nipeni maji ninywe." Ndipo wakampa siki kwenye sifongo, Naye akaikataa, na akaitema. Yeye alikuwa ni Mwana-Kondoo wa Mungu akifa mahali petu, apate kuwapatanisha wanadamu. Ilikuwa ni nini? Mungu wa Mbinguni.

301 Billy Sunday wakati mmoja alisema, ya kwamba, "Kila kijiti kilikuwa na Malaika wamekaa ndani yake, wakisema, 'Hebu vuta tu mkono ukaelekeze kidole Chako, tutabadilisha hali ya mambo.'"

302 Hilo kundi fidhuli la wenda wazimu wa kidini, linaloitwa wanachuoni fulani wenye elimu ya D.D., Ph.D., lilienda karibu

Naye na kusema, "Sasa, kama wewe ni Mwana wa Mungu! Uliwaokoa wengine; mwenyewe huwezi kujiokoa. Shuka kutoka msalabani, nasi tutakuamini."

303 Hawakujua ya kwamba walikuwa wakimsifu. Yeye angeweza kujiokoa. Lakini kama angalijiokoa, wengine asingeweza kuwaokoa. Kwa hiyo, Yeye alijitolea. Jina Lake litukuzwe. Yeye alijitoa, nipate kuokolewa nawe uweze kuokolewa. Loo, ni upendo wa jinsi gani usio na kipimo!

304 Haikumbidi kuwa mgonjwa. Huo mwili wa thamani uliozaliwa na bikira haikubidi uugue. Bali Yeye aliugua, apate kujua jinsi ya kuniombea nilipokuwa mgonjwa.

305 Haikumbidi kuchoka, bali alichoka. Nilisoma historia moja juu ya jambo hilo wakati mmoja, sijui kama ilikuwa ni ya kweli ama si ya kweli. "Wakati alipomfufua yule mvulana kutoka kule Naini, kutoka kwa wafu, Yeye aliketi juu ya mwamba na kuugua kwa kuumwa na kichwa," maana ilibidi achukuliane na magonjwa yetu.

306 Ilibidi azichukue dhambi zetu, na pale Yeye akafa, na pale Kalvari wakati yule nyuki wa kale na mauti alimdunga moja kwa moja mwiba wake. Kila mtu anajua, nyuki anapodunga kwa mwiba wake, hawezi kuchoma tena. Wakati nyuki anaporuka ama mdudu yeyote anayedunga, wakati anapodunga mwiba wake, yeye huung'oa huo mwiba. Yeye angali ni nyuki bali hana mwiba. Jambo pekee analoweza kufanya ni kuvuma na kupiga makelele chungu zima.

307 Hilo ndilo jambo pekee mauti yanayoweza kumfanyia mwamini, ni kupiga makelele sana. Lakini, haleluya, Jina la Bwana litukuzwe, Yeye aliuchukua mwiba huo wa mauti katika mwili Wake Mwenyewe. Imanueli alifanya hivyo. Akafufuka tena, katika siku ya tatu, akautoa huo mwiba mwilini Mwake, Naye ni Asiyepatikana na Mauti usiku wa leo. Na Roho Wake yumo kwenye jengo hili, Naye anajithibitisha kwamba yuko hai miongoni mwetu. Huyo ni Masihi wetu. Huyo ni Mwokozi wetu aliyetukuzwa.

*Kitabu Cha Waebrania*

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org